Jarida la Shirika la Uboreshaji Mifereji ya Asili na Uhifadhi wa Mazingira (TIP)

Maendeleo ya TIP

Toleo la 10, 2007

TIP yatia msukumo katika Kujasirisha na Uendelevu

Utangulizi

TIP ni shirika lisilo la kiselikali lililopata usajili wake tangu Agosti 1999 nchini Tanzania. Lengo kuu likiwa ni kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa progamu ya TIP mwaka 1988-2000 ili kusaidia wakulima wadogo kuboresha mifumo ya umwagiliaji asili kwa kuzingatia matumizi bora ya rasilimali ya ardhi na maji. Shirika la TIP hutoa huduma na kutekeleza mipango yake kwa kutumia kifurushi chake kifuatacho:

i. Kuimarisha vikundi vya umwagiliaji maji ili kushiriki kikamilifu katika kuboresha shughuli za umwagiliaji
ii. Kuboresha matumizi bora ya ardhi
iii. Kuboresha mifumo ya umwagiliaji asili na
iv. Kuwawezesha wakulima kuendeleza miradi ya kilimo pamoja na kukabiliana na masoko

TIP hufanya kazi maeneo yenye kilimo cha umwagiliaji asili katika wilaya nne za Lushoto (Mkoa wa Tanga), Same na Mwanga (Mkoa wa Kilimanjaro) na Arumeru (Mkoa wa Arusha) Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Vile vile TIP hufanya kazi kwa mikataba maalumu katika maeneo mengine yeyote nchini Tanzania. TIP inalenga katika kuchangia upatikanaji wa chakula na kupunguza umaskini kwa wakulima wadogo walio katika kilimo cha umwagiliaji sanjari na Mkakati wa Kukuza Uchumi Tanzania (Mkukuta) na Malengo ya Milenia

Inaendelea ukurasa wa 2

Watalamu wenza kutoka wilaya ya Mwanga wakiwa katika mafunzo

Ziara za mafunzo kwa wakulima ni njia ya kuboresha kilimo

Ziara ya mafunzo kwa wakulima wa mradi wa umwagiliji wa kijiji cha Nganjoni imeleta mabadiliko mapya. Ziara hii ni sehemu ya mafunzo ambapo wakulima 30 kutoka kijiji cha Nganjoni wilaya Moshi Vijijini walitembelea vikundi vya watumia maji vya KwaMlombola na Kwamjwi tarehe 14 Februari 2007 wilayani Mwanga kwa nia ya kujifunza mbinu mpya katika kuboresha kilimo cha umwagiliaji.

Kilichowavutia zaidi wakulima hawa ni jinsi kiasi kidogo cha maji yaliyohifadhiwa katika ndiva kinavyoweza kutumika kwa ufanisi na kuzalisha mazao mengi ya chakula na biashara. Mkulima mmoja alitoa mawazo yake na kusema kuwa Nganjoni ina utajiri mkubwa kutokana na wingi wa maji na ardhi kubwa waliyonayo.

Wakulima waliona umuhimu wa kuhifadhi maji kwenye kisima kidogo kwa kila mkulima ambavyo husaidia mgawanyo mzuri wa maji kwa wanakikundi hususani wakati maji yakiwa pungufu. Pia kilimo cha mchicha nafaka kilitoa mwamko kwa wakulima hawa. Baadhi ya wakulima walinunu mbegu za mchicha nafaka na mbegu bora ya maharage kutoka kwa Mtaalamu mwenza wa

inaendelea ukurasa wa 2

Yaliyomo

Mkutano wa wadau wa AMSDP wilaya ya Arumeru ukurasa wa **2**

Habari za wilayani ukurasa wa **3**

Kukabiliana na uhaba wa maji ukurasa wa **4**

TIP yatia msukumo katika kujasirisha na uendelevu..... *kutoka ukurasa wa 1*

Kujasirisha wakulima

Kwa muda mrefu sasa TIP hutoa huduma zake kwa wakulima wa vikundi vya umwagiliaji maji asili kupitia halmashauri za wilaya. Hata hivyo, shirika limefanikiwa kuwezesha kuwepo kwa vikundi vya wataalamu wenza katika ngazi ya vijiji. Hawa wataalamu wenza wamepewa mafunzo maalumu ya kufurushi cha TIP na wamekuwa nguvukazi muhimu na isiyo na gharama kubwa kwa TIP katika kutoa huduma.

Hivi sasa TIP inaendesha programu maalumu ya kuwaongezea uwezo wataalamu wenza walioteuliwa ili kuwawezesha kufahamu mbinu mpya, kuzitathini pamoja na kuzitumia katika kuboresha umwagiliaji. Progamu hii inategemewa kujenga kundi imara linaloaminika la washirika wa TIP ambalo litakaiwezesha TIP kutoa huduma zake kwa wakulima kirahisi na kwa gharama nafuu.

Mipango Endelevu

Kujenga uwezo wa wataalamu wenza ni kitu kinachowafaa na kitawasaidia kwenda sanjari na mabadiliko ya kimazingira katika kuboresha mbinu za umwagiliaji pamoja na matumizi bora ya maji na uzalishaji wa maji. Pia katika matumizi bora ya ardhi, masoko pamoja na mabadiliko ya mara kwa mara ya kisera za umwagiliaji, matumizi bora ya ardhi na masoko nchini. Asilimia 97% ya wataalamu wenza walioteuliwa na TIP wameonyesha kuwa wanafaa, wanauwezo na wenye kuaminika. Hata hivyo, TIP itaendelea kutoa huduma kwa kutumia watumishi wa halmashauri za wilaya kwa ajili ya usimamizi wa kitaalamu na ushauri kwa kazi za wataalamu wenza.

Matarajio

Kukuza uwezo na kutumia wataalamu wenza katika maeneo TIP inapofanya kazi kunatoa fursa ya ajira binafsi na kuunda rasilimali watu katika ngazi ya jamii waliobobea katika kuboresha kilimo cha umwagiliaji nchini. Pia huisaidia TIP kifedha, kiuchumi, kitaasisi na kijamii katika kuboresha kilimo endelevu cha umwagiliaji. Kwa ujumla huu ni mwendelezo mzuri wa sekta binafsi katika kilimo nchini.

MKUTANO WA WADAU WA PROGRAMU YA AMSDP WILAYA YA ARUMERU - GOLDEN-ROSE HOTEL 15 Februari 2007

Shirika la TIP kwa kushirikiana na Manispaa ya Arumeru liliandaa mkutano wa wadau wa Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (AMSDP) kwa wilaya ya Arumeru tarehe 15 Februari 2007 katika hoteli ya Golden Rose, Arusha.

Washiriki katika mkutano huu ni wawakilishi wa vikundi vinavyotekeleza mpango wa AMSDP wilaya ya Arumeru, Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Mtandao wa Vikundi vya Wakulima wadogo Tanzania (MVIWATA) na wadau wa ughani.

Malengo mkutano ni kuibua na kujadili kwa kina fursa zitakazowezesha shunguli za AMSDP kuwa endelevu katika wilaya ya Arumeru hususani kipengele cha pili cha programu cha **Kuwajasirisha wazalishaji pamoja na kuwaunganisha na masoko** baada ya TIP kumaliza mkataba wake

Baadhi ya mada zilizojadiliwa ni kama zifuatazo:

i Maendeleo ya mpango wa AMSDP wilayani Arumeru
ii Umuhimu wa vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS)
iii Shunguli za TCCIA na jinsi gani wakulima watafaidika nazo
iv Ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko
v Shughuli za MVIWATA na jinsi gain wakulima watafaidika nazo.

Washiriki walijadili mafanikio, changamoto na jinsi programu inavyoweza kuwa endelevu kwa kuanisha yafuatayo:

Mafanikio:

i Kuimarika kwa vikundi pamoja na mahusiano mazuri kutokana na mafunzo
ii Vikundi vinaweza kuandaa mipango kazi
iii Mafunzo ya uanzishaji Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) yamewezesha vikundi kuunda katiba, kufungua akaunti za akiba na kuanzisha mchakato wa kuandikishwa
iv Vikundi vimejenga mahusano mazuri na taasisi mbalimbali pamoja na vikundi vingine kwa nia ya kushirikishana uzoefu
v Vikundi vimefanikiwa kufanya ziara ya utafiti wa masoko katika masoko ya Kikatiti, Arusha, Kilombero na supamaketi za Masobe na Shoperite na kufanikiwa kuuza bidhaa zao kwa bei yenye faida
vi Vikundi vinapata taarifa ya masoko kwa kutumia simu za viganjani, bao za taarifa za masoko na kuamua watauza wapi mazao yao
vii Ziara za mafunzo zimewezesha vikundi kujifunza mbinu mpya katika uzalishaji, mfumo wa kuhifadhi mazao wa risiti, SACCOS na usindikaji wa mazao

inaendelea ukurasa wa 4

Ziara za mafunzo...

kutoka ukurasa wa 1

wa KwaMlombola Bw. Nzinyangwa.

Wiki mbili baada ya ziara ya mafunzo, wakulima wa Nganjoni walipanua wigo wa kilimo chao kulima mbogamboga pamoja kuiga mbinu za uhifadhi wa maji na ardhi.

Habari za Wilayani

Same

Maombi ya wakulima wa Heikeyu

TIP imewasaidia wakulima wa kikundi cha HEIKEYU katika hifadhi ya ardhi na mazingira, ujenzi wa ndiva na mfumo wa usafirishaji maji ya umwagilaji kwa njia ya mabomba kwa umbali wa mita 1000. Hii imesaidia ongezeko katika uzalishaji wa matunda, mboga mboga na viazi mviringo. Kikundi kimeomba kipatiwe mafunzo ya Kukabiliana na Masoko na Uendelezaji wa Miradi ya Kilimo ili kuwawezesha kutambua fursa za masoko yenye faida kwa bidhaa zao.

Soko la pamoja lasaidia bei ya tangawizi kupanda

TIP imetoa mafunzo ya mwangaza wa biashara kwa wakulima wa kata ya Myamba mwaka 2004. Kwa njia ya kukotoa gharama za uzalishaji na uuzaji, wakulima walichagua zao la tangawizi kama mradi wao wa kilimo. Ili kuweza kukabiliana na changamoto za bei na kuwa na lugha moja katika uuzaji, waliamua kuanzisha vituo vya kukusanyia na kuuzia tangawizi vya Myamba na Goha mwaka 2005. Vituo hivi vimewezesha bei ya tangawizi kuwa shilingi 500/= kwa kg mwaka huu. Kabla ya kuanzishwa vituo hivi bei ilikuwa sh. 250/= kwa kg

Arumeru

Barua ya Wataalam Wenza kutoka Sakaya

Sisi Wataalamu Wenza wa kikundi cha watumia maji cha Sakaya, tunapenda kutoa shukrani zetu kwa shirika la TIP kwa kutupatia mafunzo ya kutuwezesha kuwa wataalamu wenza. Mafunzo haya yametusaidia sisi kama Wataalamu Wenza na wakulima wenzetu.

Tumefanikiwa kutoa mafunzo kwa wakulima wenzetu ya kukokotoa gharama za uzalishaji kabla ya uzalishaji, hifadhi ya ardhi na mazingira na uwekaji wa kumbukumbu. Mafunzo haya yamesaidia sana kiasi kwamba wakulima wameanza kulima mazao yenye kipato kikubwa kama vile pilipili hoho, matikiti maji, nyanya na matango. Pia wamekuwa na uelewa mkubwa wa uwekaji wa kumbukumbu. Mbali na hayo tumefanikiwa kutoa mafunzo ya hifadhi ya ardhi na mazingira kwa wakulima wa kijiji cha jirani cha Manyire kata ya Mlangarini

Kilimo cha mkataba

Vikundi vya OVEGRO cha Oldonyosambu na ENDAPUKAI cha Mwandet vimefanikiwa kuingia kilimo cha mkataba baada ya kupata mafunzo. Vimeingia mkataba na kampuni AAF kwa kulima Artimisia na kampuni za maua. Kilimo hiki cha mkataba kimewapa wakulima faida kubwa kiasi cha kuboresha hali zao za kimaisha. “Kwa msimu mmoja nimepata kiasi cha shilingi 1,600.000.00 kutokana na kilimo cha artimisia katika hekta moja”.Gasper mwanakikundi wa OVEGRO

Usajili wa SACCOS

Usajili wa vikundi hufanywa ili kuvitambua kisheria vikundi vinavyofanya shughuli za kimaendeleo na katika mipango endelevu. Vikundi kumi vimepata usajili na kuwa Vyama vya Awali vya Kuweka na Kukopa (SACCOS - awali). Vikundi hivi ni OVEGRO, PAMAMA, Endavukai, Eng’arunoto, Aranga, Huduma, UWAM, Kimnyaki, MUWAKAKALE na MUVIKITA.

Hizi SACCOS - awali zitakua chini ya uangalizi wa Afisa Ushirika wa Wilaya (DCO) kwa miaka mitatu. Kwa kipindi hiki kikundi kitaangaliwa kama kinajiendesha kulingana na sheria ndogondogo walizojiwekea na kama kuna viashiria vinavyonyesha kufikia malengo yao. Mwisho wa miaka mitatu baada ya DCO kuridhika, kikundi kitapata usajili wa kuwa SACCOS kamili.

Mwanga

Mchicha nafaka

Zao la mchicha nafaka (amaranthus ssp) limeonyesha kuwa na mafanikio kwa wakulima wa Kwamlombola, Kwamjwi na Msangai. Zao hili huchukua muda wa siku 75 hadi kukomaa na halihitaji maji mengi. Katika ekari moja mkulima anaweza kuvuna kiasi cha kilo 1200. Kilo 1 huuzwa shililngi 1600. “ Zao hili ni zao lenye kipato kizuri”. Emanueli Juaeli mkulima wa Kwamlombola.

Wakulima wa mradi wa umwagiliaji wa kijiji cha Nganjoni wilaya ya Moshi vijijini wakishiriki katika mafunzo kwa vitendo ya hifadhi ya ardhi na mazingira yaliyofanyika February 2007.

TIP ni shirika lisilo la kiserikali la Uboreshaji Kilimo cha Umwagiliaji Asili na Mazingira lililosajiliwa tangu mwaka 1999. Hata hivyo shirika hili lisilo la kiserikali lililoundwa mnamo mwaka 1988, wakati ambao TIP lilianzishwa kama Mpango wa Uboreshaji Mifereji ya Asili chini ya waasisi wa shirika la Maendeleo la Uholanzi (Netherlands SNV).

TIP inashirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuweza kuwafikia kwa urahisi walengwa ambao ni wakulima wa maeneo ya umwagiliaji kwa mifereji ya asili.

Malengo ya TIP ni kuboresha na kuinua viwango vya maisha ya jamii za maeneo ya Tanzania yenye ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili, kuhifadhi maji na udongo, kustawisha misitu na maeneo ya vyanzo vya maji nchini Tanzania.

TIP inalenga kuhudumia vikundi vidogo vya wakulima (me na ke) vilivyo katika maeneo yenye umwagiliaji Tanzania.

Kifurushai cha TIP
1. Uimarishaji wa vikundi na Jinsia
2. Ushirikishwa wa Matumizi bora ya ardhi
3. Uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji
4. Kuyakabili masoko na uendelezaji wa miradi ya kilimo

Saa za Kazi
Ofisi za TIP huwa wazi
kila siku za
Jumatatu - Ijumaa
saa 2.00 asubuhi - 7:00 mchana
saa 8:00 mchana - 11:00 jioni.
Jumamosi na Jumapili pamoja na
siku za sikukuu ofisi haifunguliwi

Tuandikie
Tuma maoni yako, mapendekezo, ushauri, hadithi na mawazo yako kwa kutumia anwani ya TIP, andika jina lako kamili na anwani yako

TIP
S.L.P. Box 8909, Moshi - Kilimanjaro
Simu : 027 53025 / 54232
Faksi: 027 51124

Barua pepe: tip@tiptz.org
Tovuti: www.tiptz.org

Kukabiliana na uhaba wa maji

"Changamoto karne ya 21"

Wizara ya Maji iliandaa maadhimisho ya Wiki ya Maji kwa mwaka 2007 kweye viwanja vya Mashujaa katika Manispaa ya Moshi (mara ya mwisho maadhimisho ya Wiki ya Maji kufanyika katika Manispaa ya Moshi ilikuwa mwaka 1988)

Lengo kuu la maadhimisho ya Wiki ya Maji (kuanzia tarehe 16 - 22 Machi 2007) lilikua kutambulisha mipango ya sekta ya maji kwa umma na kuonyesha umuhimi wa kushirikisha umma katika programu za utunzaji wa mazingira na usambazaji wa maji.

TIP ilialikwa kushiriki katika maonyesho ya Wiki ya Maji ili kuadhimisha Siku ya Maji Duniani. Hii ilikuwa fursa kwa TIP kuonyesha ni jinsi gani shirika linavyohusisha miradi yake na upungufu wa maji. Maonyesho haya yalishirikisha jumla ya washiriki 50 katika makundi matatu yafuatayo:

a) Uhamasishaji na Mafunzo.
b) Biashara na wasambazaji wa bidhaa zinazohusiana na maji.
c) Huduma kwa jamii.

Siku ya kufunga maonyesho haya ambayo ni Siku ya Maji Duniani tarehe 22 March, Mgeni rasmi Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzaina Mheshimiwa Jakaya Mirisho Kikwete alitembea mabanda yote. Katika banda la TIP, rais alivutiwa sana na mchezo wa eneo bonde na maana halisi ya mchezo huo. Katika hotuba yake alisema, *"Kuna mahali nimeonyeshwa katika banda moja, wale watu wa ukanda wa chini watapigana ngumi kwa sababu ya kukosa maji"*.

Washiriki wote walishindanishwa katika makundi yao kwa vigezo vya kuelezea ujumbe wa Siku ya Maji Duniani na mpangilio wa banda. Maji Moshi Vijijini walikua washindi wa kwanza kwa jumla, wa pili Maji Ubungo na watatu Mamlaka ya Bonde la Mto Pangani.Katika kundi la Uhamasishaji na Mafunzo, National Trachoma walikua washindi wa kwanza, wa pili wakawa WAHECO –Temeke na wa tatu TIP. Kila mshiriki alipewa cheti cha kushiriki Wiki ya Maji.

Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Mh. Jakaya Mrisho Kikwete akiangalia wakati Mhandisi wa TIP Bw. Maro akitoa maelezo kuhusu mchezo wa eneo bonde ukiwa kama njia ya kuibua mijadala kuhusu mgawanyo wa maji kwa wakulima wa ukanda wa juu na wa chini wa eneo bonde la mto hasa maji yanapokua machache

MKUTANO WA WADAU..... *kutoka ukurasa wa 2*

Changamoto:

i Ucheleweshaji wa uandikishwaji wa SACCOS kumechangia vikundi kutopata mikopo kutoka mabenki.
ii Kutokua tayari kwa wafanyabiashara kuingia mikataba na wakulima.
iii Upungufu wa maghala.

Mikakati endelevu:

i Kuendela na utafiti wa masoko ndani na nje ya wilaya ya Arumeru.
ii Utekelezaji wa mipango kazi ya vikundi kama ilivyopangwa.
iii Kuendeleza mahusiano na taasisi za serikali, taasisi za kifedha, vikundi vya aina mbalimbali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi na wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji.